Tunatumia maelezo tunayokusanya ili kukupa huduma zinazokufaa, ikiwemo kukupa mapendekezo, maudhui na matokeo ya utafutaji yanayokufaa. Kwa mfano, Ukaguzi wa Usalama hukupa vidokezo vya usalama kutokana na jinsi unavyotumia bidhaa za Google. Google Play hutumia maelezo kama vile programu ambazo umesakinisha na video ulizotazama kwenye YouTube kukupendekezea programu ambazo huenda ukapenda.

Kutegemea mipangilio yako, tunaweza pia kukuonyesha matangazo yanayokufaa kulingana na mambo yanayokuvutia. Kwa mfano, ukitafuta "baiskeli za kupanda milima," unaweza kuona tangazo la vifaa vya michezo unapovinjari tovuti inayoonyesha matangazo kutoka Google. Unaweza kudhibiti maelezo tunayotumia kukuonyesha matangazo kwenye mipangilio yako ya matangazo.

- Hatutumii vigezo nyeti, kama vile rangi, dini, mwelekeo wa ngono au afya kukuonyesha matangazo yanayokufaa.
- Hatushiriki maelezo yako yanayokutambulisha binafsi kwa watangazaji kama vile jina au anwani yako ya barua pepe isipokuwa utuombe kufanya hivyo. Kwa mfano, ukiona tangazo la duka la maua lililo karibu nawe kisha uchague "gusa ili upige simu", tutaunganisha simu yako na tunaweza kushiriki nambari yako ya simu na duka hilo la maua.

---

**Nenda kwenye Mipangilio ya Matangazo**

---

## Pima utendaji

Tunatumia data kwa uchanganuzi na upimaji ili kujua jinsi huduma zetu zinavyotumiwa. Kwa mfano, tunachanganua data kuhusu mara ambazo umetembelea tovuti zetu kufanya mambo kama vile kuboresha muundo wa bidhaa. Pia tunatumia data kuhusu matangazo unayoangalia ili kuwasaidia watangazaji kujua jinsi matangazo yao yanavyosambaa. Katika kutekeleza hili, tunatumia zana mbalimbali ikiwemo Google Analytics. Unapotembelea tovuti zinazotumia Google Analytics, Google na mteja wa Google Analytics wanaweza kuunganisha maelezo ya shughuli zako kwenye tovuti hiyo na shughuli zako kutoka kwenye tovuti nyingine zinazotumia huduma zetu za matangazo.

## Kuwasiliana nawe

Tunatumia maelezo yako tunayokusanya, kama vile anwani yako ya barua pepe ili kuwasiliana nawe moja kwa moja. Kwa mfano, tunaweza kukuarifu tunapogundua shughuli za kutiliwa shaka kama vile jaribio la kuingia katika Akaunti yako ya Google kutoka mahali ambapo si pa kawaida. Au tunaweza

- Kuelewa jinsi watu hutumia huduma zetu kudumisha na kuboresha utendaji wa huduma zetu
- Kutoa huduma zinazokufaa ili kuboresha hali yako ya utumiaji
- Kutangaza bidhaa ili kuwajulisha watumiaji kuhusu huduma zetu
- Kuonyesha matangazo, hatua ambayo hufanya huduma zetu nyingi zitolewe bila malipo (na wakati tunaonyesha matangazo maalum, huwa tunakuomba idhini)
- Kugundua, kuzuia, au vinginevyo kukabiliana na ulaghai, matumizi mabaya, masuala ya usalama au kiufundi katika huduma zetu
- Kulinda dhidi ya madhara kwenye haki, mali au usalama wa Google, watumiaji wetu au umma inavyohitajika au kuruhusiwa kisheria, ikiwemo kufumbua maelezo kwa mamlaka ya serikali
- Kufanya utafiti ili kuboresha huduma zetu kwa watumiaji wetu na kunufaisha umma
- Kutimiza wajibu kwa washirika wetu kama vile wasanidi programu na wenye hakimiliki
- Kutekeleza madai ya kisheria, ikiwemo kuchunguza ukiukaji wa Sheria na Masharti yanayotumika unaoweza kutokea

## Tunapotoa huduma

Tunashughulikia data yako ili kutoa huduma uliyoomba kwa mujibu wa mkataba. Kwa mfano, tunachakata maelezo yako ya malipo unaponunua nafasi ya ziada kwenye Hifadhi ya Google.

## Tunapozingatia wajibu wa kisheria

Tutachakata data yako ikiwa tuna wajibu wa kisheria kufanya hivyo. Kwa mfano, ikiwa tunaangazia shughuli ya kisheria au ombi la kutekelezeka la kiserikali.

---

Ikiwa una maswali, unaweza kuwasiliana na Google na ofisi yetu ya ulinzi wa data. Unaweza pia kuwasiliana na ofisi ya ulinzi wa data ya eneo lako ikiwa una matatizo kuhusu haki zako kwa mujibu wa sheria za eneo lako.

---

KUHUSU SERA HII

